

Muhtasari wa ripoti ya Muungano wa Viongozi wa Afrika katika Udhhibiti wa Malaria (ALMA) | Desemba 2025

Huduma endelevu ya fedha kwa ajili huduma za afya ya msingi na afya kwa wote



Joy Phumaphi
Katibu Mtendaji
Muungano wa Viongozi wa Afrika
dhidi ya Malaria

Kadi Ya Alama Ya ALMA Kwa Uwajibikaji Na Kuchukua Hatua

Robo ya Nne 2025

→ alma2030.org/quarter-4-2025/



Utangulizi

Kipindi cha Malengo ya Maendeleo Endelevu (PHC), kimedhihirisha kuhitajika zaidi kwa mifumo jumuishi ya afya kuwa ni uti wa mgongo katika Huduma ya Afya ya Msingi (PHC). Ili kufikia lengo la Afya Kwa Wote, ufadhili wa huduma ya afya ya msingi lazima ujengwe kwenye misingi hii thabiti ya mfumo wa afya wa ndani, ikijumuisha ufadhili endelevu kutoka vyanzo vya ndani badala ya ufadhili toka nje. Nchi zinahitaji kuwa na mfumo ambao utatoa nafasi ya kifedha, kuhakikisha usawa, kuendeleza ufanisi na uwajibikaji, kwa ili kupata matokeo na kuleta athari.

Muungano wa Viongozi wa Afrika katika Udhhibiti wa Malaria - ALMA, inapendekeza matumizi ya mfumo wa mapato toka vyanzo mbalimbali. Mfumo huu unalenga katika kuhamisha mzigo wa kulipa gharama toka mfukoni mwa mtu binafsi, na kuelekezwa kwenye mfumo mmoja wa kulipia kabla ya kupatiwa huduma.

Nguzo	Eneo la Kuzingatia
Ukusanyaji wa Mapato	Kupanua Mkoba wa Afya
Kuunganisha na kushiriki hatari	Kupunguza hatari ya kifedha
Manunuzi ya Kimkakati	Kuongeza thamani ya fedha
Uwajibikaji na Usimamizi wa Fedha za Umma	Kulinda Imani ya Umma


Uhamasishaji wa Mapato: Kuunda Nafasi ya Fedha

Sehemu kubwa ya nchi zetu nyingi ni uwepo wa sekta isiyo rasmi. Hii hufanya ukusanyaji ushuru wa mapato ya kodi za kiasili kuwa mgumu. Nchi lazima kujifanyia ukaguzi katika matumizi na kuondoa kulipa ada ili kupatiwa huduma au ununuzi wa vifaa-tiba kwa ajili ya huduma kwa wagonjwa katika kituo cha kutolewa huduma za afya ya mama na mtoto na huduma nyingine za afya ya msingi. Hivyo inaleta maana kutambulisha yafuatayo:

- **Kuhama moja kwa moja kutoka kwenye muundo wa kodi na bima ya kijamii** iliyounganishwa na kulipia asilimia 0 ya gharama toka mfukoni kwa huduma muhimu za afya ya msingi.
- **Kodi za Afya (Ushuru wa Dhambi):** Kutekeleza au kuongeza ushuru kwenye tumbaku, pombe, bidhaa zenye sukari nyingi kama vile pipi na vinywaji, mafuta yenye lehemu katika vyakula. Hizi ni sera za kufanikisha ushindi maradufu ambazo zinazalisha mapato huku zikipunguza mzigo wa magonjwa yasiyoambukiza.
- **Ushuru wa Ubunifu:** Tozo ndogo, za kielektoniki kwenye mawasiliano ya simu (Kama vile ada ya dola 0.01 kwa kuhamisha pesa kwa njia ya simu), zinaweza kuzalisha mapato makubwa yanayotabirika kwa ajili ya huduma ya afya ya msingi.
- **Deni la kubadilishana Afya:** Hili linahitaji nchi kujadiliana na wakopeshaji ili kuelekeza upya ulipaji wa riba kwenye mikopo, kwa miundombinu ya ndani na programu za huduma ya afya ya msingi.
- **Ufadhili Mseto:** Kuondoa hatari ya uwekezaji binafsi kwenye sekta ya afya ambao unachanganya rasilimali kutoka sekta ya umma, wafadhili na sekta binafsi. Mifano ni kutumia majengo ya serikali ya kutolea huduma na kuyakodisha kwa sekta binafsi.
- **Mabaraza na Mfuko wa Afya wa Taifa:** Mabaraza na mifuko ya kutokomeza malaria yameonesha kuwa ushirikiano wa ufadhili kati ya serikali na sekta binafsi


wenye mpangilio mzuri na wadau muhimu wa afya na sekta binafsi, ambapo watakuwa na sauti, uhibiti na uangalizi sio tu katika kukusanya rasilimali, bali pia kuhakikisha wanafikia malengo, ufanisi na matokeo, kipaumbele kwa huduma ya afya ya msingi.

Mabaraza yaliyopo, ambayo yalianzishwa kwa kuwaleta wadau pamoja katika kampeni ya Ziro Malaria Inaanza na Mimi, sasa yanafanya kazi katika nchi 9 na mabaraza yameanzishwa katika nchi sita. Tayari wamekusanya zaidi ya dola za kimarekani milioni 200. Fedha hizo zinaweza kutumika kutekeleza mpango wowote wa afya, kutegemeana na kipaumbele. Kuanzisha mfuko mmoja wa afya wa kitaifa, na uangalizi wa pamoja kwa kushirikisha sekta ya umma/binafsi ni muhimu katika utoaji huduma za afya na mwitikio wa haraka inapotokea milipuko wa magonjwa.



Chanzo: Robo ya 4 ya mwaka 2025 - Kadi ya Alama ya ALMA

Mabaraza na Mifuko wa Kutokomeza Malaria na Magonjwa ya Kitropiki ambayo yaliyokuwa hayapewi kipaumbele



Chanzo: Robo ya 4 ya mwaka 2025 - Kadi ya Alama ya ALMA

Uzinduzi wa Ziro Malaria Inaanza na Mimi

Kuunganisha na Kupunguza Hatari

Hii inahusisha kutambua kuwa afya ina mambo mengi na kwamba viashiria vya afya viko katika kila sekta, hivyo kuhitajika ushirikiano katika jukumu la kudhibiti kuugua, na kuzuia kuenea kwa magonjwa; ni njia yenye mantiki katika sekta mbalimbali za serikali.

Kwa mfano, jukumu la Wizara ya Mazingira na Kilimo katika kudhibiti athari za mabadiliko ya tabianchi na kuongeza uzalishaji wa chakula kwa kupunguza maeneo ya mazalia ya wadudu dhurifu kama vile mbu waenezo malaria; kuanzisha na pamoja na kufadhili programu za uhibiti wa vekta ni mfano mzuri wa jukumu hili la pamoja.



Chanzo: Robo ya 4 ya mwaka 2025 - Kadi ya Alama ya ALMA

Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Magonjwa Yanayosababishwa na Vekta katika Michango Iliyoamuliwa Kitaifa

Ununuzi wa Kimkakati

Hatari hii ya pamoja inaenea kwa namna ambayo ugawaji rasilimali na ununuzi wa kimkakati unafanywa na sekta zote, ikijumuisha sekta ya afya.


Sekta zote zinatakiwa kufuatilia kuhusu rasilimali; je, zinatumika kufanya nini, kiasi gani kinatumika, na jinsi kinavyotumika.

- **Malipo Kwa Kichwa:** Badala ya kulipa/kuwapatia kliniki kiasi cha dola kulipia gharama ya kila kidonge kinachotolewa, serikali inaweza kulipa kiasi maalum kilichopangwa kwa kila mtu katika jamii, na kuweza kuzuia afya kwa ufanisi. Hii inawapa motisha watoa huduma za afya ya msingi na kuziweka jamii zao zikiwa na afya bora, badala ya kusubiri mpaka waugue.
- **Zingatia Kanuni ya "Huduma ya Afya ya Msingi-Kwanza":** Nchi zinapaswa kuamua kisheria kwamba asilimia maalum (m.f., 50%) ya bajeti ya afya ya kitaifa itengewe kwa ajili ya huduma za afya za msingi. Aidha, ni lazima kuwe na asilimia zilizowekwa

kwa sekta zinazohusiana ili kuweka uzio kwenye sehemu ya bajeti zao kwa ajili ya huduma za afya za msingi. Huduma duni za afya ya msingi husababisha mzigo mkubwa wa huduma kuhamishiwa kwenye hospitali za rufaa na hospitali zinazotoa huduma za kibingwa.


- **Ufadhili kulingana na Matokeo (PBF):** Hii inaweza kupangwa ili kuongeza manufaa kwa wafanyakazi wa kliniki ambao wanafikia malengo ya maendeleo endelevu. Malengo ya kikanda na kitaifa, na kuimarisha programu mahsusi za mfumo wa afya.

Kwa mfano, nchi zimeshauriwa wakati wote kuwa na akiba ya dawa mseto na vitendanishi kwa matumizi ya angalau miezi 3, ili kuhakikisha kuwa milipuko ya malaria haitokei pasina kudhibitiwa. Ramani zilizo hapo chini zinaonesha nchi nyingi kushindwa kukidhi hitaji hili muhimu, ambalo linaweza kuokoa maisha ya maelfu kila mwaka.



Chanzo: Robo ya 4 ya mwaka 2025 - Kadi ya Alama ya ALMA


Akiba ya Dawa Mseto za Malaria zilizopo
(zaidi ya miezi 6)



Chanzo: Robo ya 4 ya mwaka 2025 - Kadi ya Alama ya ALMA

Akiba ya Vitendanishi iliyopo
(zaidi ya miezi 6)

- Zaidi ya hayo, idadi kubwa ya nchi bado hazijatia saina na kuridhia Hati za Wakala wa Dawa wa Afrika (AMA) katika Tume ya Muungano ya Afrika (AUC), ambazo zingeimarisha Wakala wa Dawa wa Afrika, na kuruhusu nchi kunufaika kutokana na ununuzi wa bidhaa kwa wingi na kupunguzwa bei ya manunuzi kutokana na ununuzi wa pamoja, ikiwemo kuboreshwa kwa usimamizi wa ugavi.





Chanzo: Robo ya 4 ya mwaka 2025 - Kadi ya Alama ya ALMA

Kusaini na Kuridhia Hati ya Wakala wa Dawa wa
Tume ya Muungano ya Afrika

Ufanisi katika Uendeshaji & Uwajibikaji na Usimamizi wa Fedha za Umma (PFM)



Uwajibikaji katika Usimamizi wa Fedha za Umma (PFM) unahitaji viongozi katika ngazi zote, kuhakikisha usimamizi wao wa fedha za umma, kuhakikisha uwazi, ufanisi, na thamani ya fedha katika matumizi ya rasilimali.

- Nchi zinahimizwa kutumia takwimu zilizokusanywa katika muda halisi kupitia mifumo ya taarifa za usimamizi wa afya, ili kujaza zana za usimamizi wa kadi za alama zinazotupatia taarifa ili kufanya maamuzi na kupima maendeleo ya utendaji na matokeo.
- Huduma za afya za msingi zilizojumuishwa ni muhimu sana. Hii itahusisha kuunganisha chanjo ya malaria na huduma zingine katika utaratibu wa kawaida, na kinga ya madhara ya malaria kwa mjamzito kipindi kabla ya kujifungua, na matibabu ya malaria katika usimamizi jumuishi wa wagonjwa katika ngazi ya jamii.



Chanzo: Robo ya 4 ya mwaka 2025 - Kadi ya Alama ya ALMA

Utekelezaji wa Chanjo - DPT3 mwaka 2024 (Chanjo watoto miezi 0-11)



Chanzo: Robo ya 4 ya mwaka 2025 - Kadi ya Alama ya ALMA

Kuanza Kutumika kwa Chanjo ya Malaria

- Uwekaji Huduma za Afya ya Msingi Kidijitali: Utekelezaji wa rekodi za afya za kielektroniki kwa huduma za afya toka sekta zote za afya za umma na za binafsi kuanzia ngazi ya huduma za msingi hadi hospitali za rufaa, hupunguza upimaji wa marudio na matumizi mabaya ya dawa; pamoja na usugu wa dawa za antibiotiki (AMR). Hii inaweza kuokoa hadi asilimia 20 ya gharama za uendeshaji.

Utaratibu wa kidijitali lazima ujumuishe utekelezaji wa mfumo wa ufuatiliaji wa kidijitali wa dawa na vifaa-tiba, kwa kutumia Akili Bandia katika kukisia mahitaji na usimamizi wa ugavi.

- Kuunganishwa kwa Wahudumu wa Afya ngazi ya Jamii (CHW) na kurasimisha Kada ya Wahudumu wa Afya ya Jamii wanaolipwa. Wahudumu wa Afya ya Jamii ni njia ya gharama nafuu zaidi ya kutoa huduma ya kinga, kupunguza huduma ya kliniki zenye gharama, na kuhudumiwa katika chumba cha wagonjwa wa dharura.

Hitimisho

Enzi za utoaji huduma za afya zinazotegemea misaada ya maendeleo kwa nchi zinazoendelea - ODA / wadau zinafikia mwisho. Nchi zinajipanga kulinda huduma ya afya ya msingi na kutumia fursa hii, ili kuimarisha mifumo ya huduma za afya ya msingi kwa njia endelevu, na kuharakisha maendeleo kuelekea malengo ya maendeleo ya endelevu na Afrika tunayoitaka.

Uteuzi na namna ya nyenzo zilivyowasilishwa katika ramani hizi, hauna uhusiano wowote na maoni ya uongozi wa ALMA kuhusiana na hadhi ya kisheria ya nchi yoyote, eneo au eneo la mamlaka yake au kuhusu uwekaji mipaka au mipaka yake.